# Fasihi Simulizi kama Nyenzo Muhimu katika Taaluma ya Kitabibu (Afya)

*Neema Julius Luhwago*
*Chuo Kikuu cha Dodoma*

**Ikisiri**

**Lengo la makala haya ni kueleza jinsi fasihi simulizi ilivyo nyenzo muhimu katika taaluma ya kitabibu kwenye uelimishaji na kuitahadharisha jamii kuhusu magonjwa kama vile; UKIMWI, UVIKO-19, Kaswende, Kisonono, Saratani, Kifua kikuu na Malaria. Aidha, unaweka bayana namna taaluma ya kitabibu inavyoweza kutumia fasihi simulizi katika kuwasilisha ujumbe wa elimu ya magonjwa kwa urahisi. Utafiti wa makala haya ni wa kitaamuli. Data za makala haya zimekusanywa uwandani na maktabani ambapo mbinu ya mahojiano na uchambuzi matini zilitumika. Mjadala wa utafiti umeongozwa na nadharia ya Wanasosholojia iliyoasisiwa na Bronislaw Malinowsky, A.R Radclife Brown na Franz Boaz. Waasisi wa nadharia hii walivutiwa sana na fasihi simulizi kwa kuzingatia upekee wa kimuktadha kwa kila jamii. Msingi mojawapo wa nadharia hii ni kuyatazama masuala mahususi katika jamii hususani tanzu za fasihi simulizi na dhima zake. Matokeo ya utafiti wa makala haya umeonesha kwamba taaluma ya fasihi simulizi na kitabibu (afya) zinaweza kushirikiana katika harakati mbalimbali za kuielimisha na kuitahadharisha jamii kuhusiana na magonjwa kwa kutumia misemo, maigizo, mazungumzo na nyimbo ili kurahisisha ufikishwaji wa ujumbe na elimu ya masuala ya afya kwa jamii husika.**

**Maneno Muhimu**: *Fasihi Simulizi, Nyenzo, Taaluma ya Kitabibu*

**Utangulizi**

Wanataaluma mbalimbali na wadau wa fasihi wameweza kuijadili fasihi simulizi katika mitazamo tofauti tofauti katika kutoa fasili ya fasihi simulizi. Baadhi yao ni kama wafuatao: Okpewho (1992) anasema fasihi simulizi ni matini ya kiubunifu ambazo huvutia fikra zetu au hisia au mihemko. Tanzu zake ni michezo ya kuigiza, hadithi na mashairi. Naye Mrikaria (2007) anaielezea fasihi simulizi kuwa ndio fasihi kogwe iliyoanza tangu binadamu alipoanza kutumia lugha kama chombo cha mawasiliano. Hapo ndipo mwanadamu alipoanza kutumia nyimbo, methali, vitendawili, maigizo na hadithi katika kufikisha ujumbe kwa wanajamii ikiwa ni kwa kuonya, kuelimisha au kuburudisha. Aidha, urithishwaji wa mila na desturi kutoka kizazi kimoja kwenda kingine ulifanyika.

Mulokozi, M (1996:24) anafasili kuwa ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa mdomo na vitendo bila kutumia maandishi. Kimsingi fasihi simulizi ni Tukio (si dhana) linalofungamana na muktadha wa kijamii na hutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita: fanani/msanii, hadhira, fani inayotendwa, Tukio, mahali/mandhari na wakati. Pia Njogu (2006) anatoa msisitizo katika fasihi simulizi kuwa na ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa ya kuibua mitazamo mbalimbali katika jamii kuhusu uchumi, siasa na mila na desturi. Upekee na uhai wa fasihi simulizi huletwa na tanzu zake kutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao ya kila siku. Wanajamii hutumia nyimbo, hadithi, mashairi na michezo mbalimbali katika kuburudika, kuelimishana na kuhusiana.

Okot P'Bitek (1973:20) fasihi simulizi hujumuisha tanzu zote za matumizi ya lugha ya kubuni zenye kutumia maneno kwa njia ya kitamathali au kimafumbo ili kuwasilisha hisia na fikra za mwanadamu. Wataalamu wote hawa wanajadili kuwa fasihi simulizi ni lazima itungwe na kuhifadhiwa kichwani na pia iwasilishwe kwa njia ya mdomo.

Kwa mitazamo hiyo, makala haya yanaona kuwa fasihi simulizi ni sanaa ya lugha inayobuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia mbalimbali ikiwemo mifumo ya kielektroniki. Hii imetokana nakuona kwamba fasili nyingi za wataalamu mbalimbali zinaifasili fasihi simulizi kwa mtindo wa kimapokeo usiotazama upya wowote unaotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwani fasili hizo hazizungumzii lolote kuhusu matumizi ya vyombo vya kisasa vya sayansi na teknolojia katika kubuni, kutongoa na kuhifadhi fasihi husika. Baadhi ya vyombo ni kama vile, Radio, Video, DVD, VCD, Runinga, Kompyuta na Wavuti ambavyo kwa sasa vinatumika katika kutolea na kurekodia tanzu za Fasihi Simulizi kama vile hadithi, nyimbo, maigizo, vitendawili, semi n.k.

**Kiunzi cha Nadharia**

Katika tafiti za kitaaluma, ufafanuzi wa data za kitafiti hujiegemeza katika nadharia fulani ili kuhalalisha na kurahisisha uelewekaji wa mada ya utafiti. Nadharia ni mawazo, maelekezo au mwongozo katika kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Aghalabu nadharia huwa kama nyenzo ya kutusaidia ili tufikie lengo fulani. Hata hivyo kila nadharia huwa na udhaifu na ubora katika kuelezea hali au tukio fulani. Tunaweza kujumuisha kuwa nadharia ya fasihi simulizi ni nyenzo inayotoa mwongozo kuhusu mwelekeo wa jamii fulani.

Makala haya yametumia nadharia ya Wanasosholojia iliyoasisiwa na Bronislaw Malinowski (1945), A.R Radclife Brown (1947) na Franz Boaz (1942). Waasisi wa nadharia hii walivutiwa sana na fasihi simulizi kwa kuzingatia upekee wa kimuktadha kwa kila jamii. Msingi wake ukiwa ni kuyatazama masuala mahususi katika jamii hususani tanzu za fasihi simulizi na dhima zake. Raghba kubwa ya waasisi na wafuasi wa nadharia hii ilikuwa kutoka katika masuala ya kiutamaduni na kuingia katika masuala ya kijamii. Hawa waliona kuna haja ya kuangalia masuala mahususi zaidi ya kijamii, na siyo kufanya masuala ya kijumla jumla. Ukilenga katika masuala mahususi inasaidia kuleta urahisi wa kuona tofauti kati ya jamii moja na nyingine. Pia ililenga kuangalia tofauti kuliko mfanano, hivyo walijaribu kila namna ili kuona upekee wa kila jamii, kwa mfano desturi za jamii na tofauti zake. Walichunguza kila jamii kwa kuzingatia upekee wake kimazingira na walirekodi vipera mbalimbali vya tanzu za fasihi simulizi kama vile ushairi, ngano, methali n.k. Aidha, nahdaria hii inaondoa mtazamo uliokuwa umedhaniwa hapo mwanzo kuwa fasihi simulizi ni mabaki tu ya zamani na kwamba hayakuwa na umuhimu wowote katika jamii za kisasa. Hivyo waliamini kuwa uamilifu wa fasihi simulizi uko hai na haufi na kwamba hubadilika kulingana na maendeleo ya jamii husika.

Kutokana na msingi wa nadharia hii ya sosholojia makala haya yatajikita katika ufafanuzi wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi na dhima zake kwa jamii na jinsi zinavyohusiana na taaluma ya kitabibu. Vilevile, kujikita katika utumizi wa tanzu husika katika mawasiliano ya wanajamii hususani katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

**Methodolojia ya Utafiti**

Data za makala haya zimekusanywa kwakutumia mbinu ya mahojiano na uchambuzi matini. Mbinu hizi zimechaguliwa kwasababu ya umuhimu wake katika uchambuzi wa tanzu za fasihi simulizi hasa katika masuala yanayoihusu jamii. Mbinu hizi hutumika kwa lengo la kuchunguza, kuelewa, na kubaini jinsi semi, nyimbo, maigizo, masimulizi na mazungumzo, nahau na methali zinavyotumika katika kuelimisha jamii kuhusiana na magonjwa kama vile malaria, UKIMWI, UVIKO -19, saratani na mengineyo. Aidha, data za utafiti huu zimepatikana kutoka kwa wanataaluma, wadau mbalimbali wa Kiswahili na wanazuoni wa vyuo vikuu mbalimbali nchini Tanzania hususani UDSM, UDOM, ST. JOHN'S university pamoja na raia wa kawaida. Maeneo haya yamechaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kwa kuwa ni maeneo ambayo yana kundi kubwa la watu lililopamoja na hupendelea kutazama televisheni na kujadili yanayowasilishwa. Utangamano huo katika maeneo hayo umesababisha wadau na wanazuoni hao kuwa na taarifa nyingi za misemo, methali, maigizo, masimulizi na nyimbo ambazo zinarushwa kwenye TV na kuwaelimisha kujiepusha na magonjwa ambukizi hususani UKIMWI nakadhalika. Kwa hivyo basi, sampuli tajwa hapo juu imesaidia katika upatikanaji wa data zilizofanikisha utafiti wa makala haya.

**Fasihi Simulizi na Taaluma ya Kitabibu (Afya)**

Taaluma ya kitabibu ni elimu inayoshughulikia au kujihusisha na utoaji tiba na tahadhari kuhusuafya za viumbe hai hususani binadamu. Wizara ya afya nchini Tanzania ndio inayohusika na masuala ya afya na maendeleo yake, ikiwa imeunda idara mbalimbali. Idara ya Kinga na elimu ya afya ina jukumu la kutoa huduma bora za kinga pamoja na elimu ya afya kwa wananchi ili kujikinga na

maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Uhusiano wa fasihi simulizi na taaluma ya kitabibu unajipambanua zaidi katika tanzu za fasihi simulizi kupitia dhima zake na ujumbe unaowasilishwa.

Tukiirejea historia ya fasihi simulizi tunaona babu zetu walitumia hadithi, maigizo, misemo, methali, nahau, vitendawili na nyimbo katika kufikisha ujumbe wa ushauri na mafunzo mbalimbali kama vile jando, unyago na tiba za jadi. Kwa mfano jamii ya waswahili katika shughuli za jando na unyago walitumia "*nyimbo"* (nyiso) hizi ni nyimbo zinazohusiana na tohara. Baadhi ya jamii nyingi za Kiafrika zilithamini sana tohara hususani kwa wavulana. "*Nyiso"* ziliimbwa kwa dhumuni la kuwakusanya pamoja na kuwapa moyo watahiriwa, kuwaondoa hofu na woga, kuwatayarisha watahiriwa ki-hisia ili kukabiliana na kisu cha ngariba kwa ujasiri na kuuaga utoto na kuingia katika utu uzima. Mfano mwingine ni nyimbo za kuchapusha kazi "*chapuzo*" nyimbo hizi ziliimbwa ili kuwahamasisha wanajamii katika kazi maalumu wanayoifanya na kuondoa uchovu. Mfano jamii ya waswahili ina nyimbo kama "*Wawe*" hizi ni nyimbo za kuchapusha kazi za wakulima na "Kimai" hizi ni nyimbo za kuchapushakazi za wavuvi na mabaharia.

Pia katika tiba za jadi, hapo wanzo jamii zilitumia wazee wakongwe wenye uzoefu wakupambana na majanga mbalimbali ya magonjwa yaliyoibuka katika jamii zao, hivyo kusababisha kuibuka kwa waganga wa jadi waliotumia mitishamba, mizizi na mikojo ya wanyama kuweza kutibu wagonjwa. Kwa mfano, jamii ya Wahehe wapatikanao katika mkoa wa Iringa nchini Tanzania hutumia baadhi ya mizizi na matunda pori kama vile "*vitowo"* ambavyo ni aina ya matunda mwitu yenye utelezi kama bamia ambayo hutumika kwa mtu ambaye amefunga choo hupewa matunda hayo na kutokana na utelezi wake anapoyala kwa wingi humsaidia kupata choo. Pia jamii hii ina matunda yanayoitwa "*misasati"* ambayo ina muwasho mdomoni mithili ya pilipili iliyochanganywa na tangawizi na limao. Matunda haya jamii hii huamini kuwa yanasaidia kutibu kikohozi na mfumo wa hewa kwa jumla hasa pale mgonjwa anapoyala kwa bidii. Vilevile katika suala la ulinzi na usalama, jamii ilitumia michoro ya picha mbazo zilionyesha ni aina gani ya Wanyama wanapatikana katika eneo husika. Kwa mfano jamii wa ya Warangi kutoka Kondoa Irangi nchini Tanzaniakatika mkoa wa Dodoma wana eneo la michoro ya kale ya mapangoni ambayo ilichorwa na watu wa zamani kwa kutumia damu za wanyama. Michoro ila haiku katika mapango tuu bali hata katika miamba yam ilima pembezoni mwa njia inaonekana na historia ya wenyeji inaonyesha kuwa wazee wa zamani waliichora ili kuwasiliana kwa kutumia picha za wanyama kumtaarifu mwenzake anayepita hapo kuwa eneo hilo lina Wanyama wa aina gani hususani kwa wawindaji. Imechorwa michoro ya simba, swala, twig ana wengineo. Hivyo, tunaona mawasiliano ya kutumia picha na michoro yalikuwepo tangu enzi za mababu zetu. Katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia ni mabadiliko tu ya michoro kuwa katika mabango, picha kuchorwa kwa kutumia rangi mbalimbali zilizotengenezwa viwandani, picha kubandikwa katika mabango maalumu au kurushwa katika vyombo vya habari kama televisheni (runinga). Jambo hili linadhihirisha wazi kuwa fasihi simulizi imepiga hatua kimaendeleo na inaenda na wakati ambao jamii husika imeufikia.

**Fasihi Simulizi kama Nyenzo**

Kamusi kuu ya Kiswahili (2016), inaeleza kuwa nyenzo ni kitu ambacho hutumiwa kutengenezea kitu kingine au kukamilisha mahitaji ya kitu kingine. Makala haya yanafasili nyenzo kuwa ni uwezo wa kitu kukamilisha mahitaji ya kitu kingine. Ukamilisho huo katika fasihi simulizi na taaluma ya kitabibu unajidhihirisha kupitia tanzu za fasihi simulizi ambazo ni mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi, semi kama vile methali, nahau na lakabu. Ufafanuzi wake ni kama ufuatao:

**Semi**, ni utanzu wa fasihi simulizi unaotumia lugha fiche iliyobeba maana nzito inayohitaji ufafanuzi. Semi huweza kuwa zile zinazozuka na kudumu kwa muda mrefu na zingine kwa muda mfupi. Zile zinazozuka kwa muda mfupi huitwa misimu ambapo huzuka na kupotea kutokana na mud ana mazingira. Mifano ya misemo kama vile "*kuugua si kifo*" msemo huu unapotumika huweza kumtia moyo mgonjwa hata kama ana hali mbaya. Pia hata kwa watu wasio wagonjwa huweza kupata matumaini pale ambapo siku za usoni wanaweza kupatwa na magonjwa au watu wao wakaribu wakipatwa na magonjwa kujua kuwa kupatwa na ugonjwa au kuugua si kufa bali ni ugonjwa unaoweza kutibika au tatizo linaloweza kukabilika na kupatiwa ufumbuzi.

"*Mtu ni Afya*" msemo huu huweza kumtia moyo mtu kuilinda afya yake na kuchukua tahadhari stahiki. Kuna misemo kama vile *"Malaria haikubaliki*" msemo huu umekuwa ukirushwa kwenye runinga na umekuwa ukijenga tafakuri kwa wanajamii kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kutumia chandarua chenye dawa ya kuzuia mbu. Nchini Tanzania katika uongozi wa awamu ya nne ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliweza kuonekana katika runinga kwa tangazo fupi akisisitiza kwa kusema "*Malaria Haikubaliki*". Yeye kama kiongozi wa nchi na mamlaka aliyonayo iliwafanya wananchi wa Tanzania kuchukua tahadhari nah atua stahiki zakuweza kupambana na ugonjwa wa malaria na hatimaye kupunguza kasi ya ueneaji wa ugonjwa huo. Pia kupambana na utokomezaji wa visababishi vya ugonjwa huu kama vile kufyeka majani yaliyo karibu na makazai, kuchoma moto taka, kufukia madimbwi ya maji n.k. Vilevile katika kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19 baada ya kugundulikwa kwa chanjo ambapo mbiu ilipigwa dunia nzima watu kuchanja ikiwemo nchi yetu ya Tanzania. Katika harakati mbalimbali za kuhamasisha wananchi kuchanja iliibuka misemo mingine mingi kama vile "*Ujanja kuchanja*:" Kuna msemo kama "*Mkono sweta*" ni msemo uliotumiwa na idara ya kinga na elimu ya afya katika kampeni za kutolea mafunzo kwa Wanaume kuhusu tohara hasa wale ambao tayari ni watu wazima lakini hawakufanyiwa tohara. Msemo huu ni wa lugha ya ufiche iliyobeba maana ambayo ni lazima imtafakarishe msilikizaji au msomaji wa mabango yaliyokuwa yamebandikwa kutangaza kampeni hiyo bila kumdhalilisha Mwanaume kwa kutaja viungo vyake vya uzazi ambavyo havijafanyiwa tohara. Vilevile methali ni miongoni mwa kipera cha semi ingawa kuna wataalamu wengine wa fasihi huona kuwa ni utanzu unaojitegemea Katika makala haya tunaufafanua kama kipera cha semi kutokana na maana yake.

**Methali** ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na tajriba ya jamii husika. Methali huwa na maana ya juu na ya ndani zaidi ambayo huweza kupokezanwa kutoka kizazi kimoja na hadi kingine. Aghalabu methali huwa na mpangilio wa manenoambao hudhihirisha pande mbili za fikra; upande mmoja huonyesha hali na upande wapili huonyesha matokeo a tendo hilo au sharti. Aidha, kuna aina nyingi za methali, miongoni mwazo ni zile zinazoonyesha falsafa mbalimbali za Maisha ya jamiihusika na zingin ni zile zinazo onya, kushauri au kutia moyo. Kuna methali kama vile "*Mficha maradhi kifo humuumbua"* kwa fasili ya wazi ya methali hii tunaona kuwa imebeba funzo linaloitahadharisha jamii kutokukaa na maradhi bila ya kwenda kwenye vituo vya afya ili kupata matibabu. Wanajamii wanaaswa kuwa wasipotibiwa mapema kifo kitakapofika hakitafichika. Mfano mwingine ni *"Mficha uchi hazai"* methali hii inaonyesha jinsi ambavyo mwanamke akiwa anataka kuzaa nilazima afunue uchi wake ili kuweza kusaidika na mtoto kutoka. Akiona aibu ya kuzifunua sehemu zake za siri kwa wakunga hataweza kuzaa. Vilevile suala la uzazi ni sualalinalohusisha kujamiiana kati ya mwaume na mwanamke. Tendo la kujamiiana linahusisha via vya uzazi (uchi). Tukio hili huweza kutokea kwa mtu hususani mwanamke akiwa na aibu ya kuto kuufunua uchi wake ili kujamiiana hawezi kupata mimba na hatimae kuzaa.

Pia **lakabu** zinajipambanua katika utanzu wa semi kuwa ni majina yakupanga ambayo baadi ya watu hupewa kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimwenendo. Baadhi ya majina hayo huweza kuwa ni ya kumkosoa mtu au hata kumdhalilisha kutokana na tabia au matendo yasiyokubalika katika jamii anayoyatenda au kunasibishwa nayo. Kwamafano msemo kama vile "*Mchepuko siyo dili baki njia kuu*" msemo huu umebeba lakabu '*Mchepuko'* inayomaanisha mpenzi wa siri(mwanamke au mwanaume) ambaye si mwenzi wa ndoa, wengine huita nyumba ndogo au *kimada* kwa mwanamke. Msemo huo unaaibisha na kuwadhalilisha watu wote walio na *michepuko* kwa kuonyesha kuwa si jambo lenye maana au tija, si jambo au tabia nzuri bali ni ushenzi na kujiingiza katika matatizo. Aidha, unaelezea kuwa ni heri kutulia na mwenzi wako (mpenzi)mmoja mwaminifu na kuendelea kuwa salama. Msemo huo wa Mchepuko siyo dili umekuwa ukitumiwa sana na wadau wa afya katika kuitahadharisha jamii kuhusu madhara ya kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja na kushirikiana nae masuala ya ngono inayochangia katika maambukizi ya magonjwa hatarishi kama vile; *UKIMWI(HIV), Kaswende, Kisonono, Pangusa, Homa ya Ini B (Hepatitis B)* na mengineyo yanayo weza kuenea kupitia ngono. Kupitia matangazo katika vyombo vya Habari hususani televisheni(runinga), michoro ya picha, na vibonzo mbalimbali, wizara ya afya au wataalamu wa afya wanaweka mkazo kwa wanajamii kutulia na kushirikiana na mwenzi wake(mpenzi) tendo la ndoa ili kupunguza kasi ya maambukizi ya maradhri yanayoenea kupitia ngono. Hivyo basi, katika utanzu huu

wa semi tunaona namna ambavyo taaluma ya kitabibu inavyoweza kutumia semi katika kuielimisha, kuionya na kuitahadharisha jamii kuhusu magonjwa mbalimbali.

**Maigizo au drama** ni utanzu ambao hutumia watendaji kuiga matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani. Katika utanzu huu tunaona mifano ya michezo ya kuigiza kama vile "FATAKI" unaorushwa kituo cha taifa cha kurushia matangazo (TBC), hutoa tahadhari kuhusu maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI hususani kwa vijana kujiepusha na vishawishi na utapeli wa kimapenzi. Pia nchini Kenya, mchezo wa kuigiza wa "*Mama Kayai na Baba Kayai*" uliokuwa ukiongozwa na msanii maarufu marehemu Mzee Ojuang katika kipindi cha Vitimbi kinachorushwa na Kenya broadcasting Corporation (KBC Chanel) Wasanii hawa wakiongozwa na marehemu Mzee Ojuang walitumia maigizo kuionya jamii kuhusu masuala mbalimbali hususani magonjwa hasa ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake kwa jamii.Kupitia mchezo huo wa kuigiza tunaona jamii yote ya Wakenya na Afrika mashariki kwa jumla iliweza kupata elimu ya kijikinga na kuchukua tahadhari.

Vilevile kuna filamu mbalimbali ambazo zimeigizwa kwa madhumuni ya kutolea mafunzo yahusuyo afya kwa wanajamii.

Kwa mfano: Idara ya Kinga na elimu ya afya Zanzibar katika ripoti yao ya afya ya mwaka 2014 ilisema "kumekuwa na juhudi mbali mbali zinazofanywa ili kukuza uwelewa wa jamii juu maradhi yasiyoambukiza, mojawapo ni filamu maalum iliyoandaliwa yenye kueleza mambo hatarishi yanayochangia katika kupata maradhi haya. Filamu hii imetayarishwa kwa kushirikiana na idara ya habari maelezo na kuionesha katika vijiji mbali mbali vya Unguja. Pia vipindi mbali mbali vya runinga na redio kuhusiana na lengo hilo vimerushwa hewani".

Vilevile, katika taasisi za elimu ya juu hususani vyuo vikuu kama Chuo Kikuu cha Dodoma kumekuwa na matamasha mbalimbali yanayoonesha michezo ya kuigiza jukwaani yaani drama kama vile "Kilio Chetu" ni tamthiliya iliyobeba maudhui ya kuifunza jamii husasani vijana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake kwa kuepukana na vishawishi na ngono zembe. Kupitia makongamano mbalimbali ya wanafunzi katika jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dodoma, maigizo na vichekesho vimekuwa vikitolewa makusudi kwa lengo la kuendelea kuikumbusha na kuitahadharisha jamii kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI. Kupitia utanzu huu wa maigizo tunaona ukamilishano uliopo kati ya taaluma ya kitabibu na fasihi simulizi kwani uigizaji unaeleweka zaidi kuliko kutumia lugha ya sayansi ya kitabibu ambayo inaeleweka kwa waliosoma sayansi hiyo ya kitabibu.

**Nyimbo**, ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi, wimbo huwa ni utungo ambao una mpangilio maalumu wa maneno na una mahadhi. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu kadhaa. Nyimbo huhusisha maneno kuhusu jambo fulani na sauti ya mwimbaji.

Nyimbo zimeenea sana miongoni mwa jamii mbalimbali na huimbwa kuambatana na shughuli mbalimbali ili kuwatia moyo katika kazi zao na hutumika pia kuelimisha jamii masuala ya afya. Kwa mfano, wimbo wa "*Starehe"* ulioimbwa na msanii Ferouz na nyimbo mbalimbali zinazoimbwa na wasanii kwenye maadhimisho ya siku ya madawa ya kulevya, UKIMWI, uhamasishwaji wa uchanjaji wa chanjo ya UVIKO-19. Wasanii kama vile Wasafi na Diamond na wimbo wa "*Quarantine*", Mrisho Mpoto na wimbo wake wa "*Kwaheri Corona*" Wimbo huo umejaa maelekezo ya namna ya kupambana na UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na kuelekeza kuhusu kufanya mazoezi, kutumia tangawizi, kufukiza nyungu na kula vyakula vinavyoongeza kinga ya mwili. Mfano mwingine ni wimbo wa Salome Waimiru unaoitwa "*Janga la Corona*" msanii huyu ameimba kwa hisia za huzuni hali akionyesha hatua stahiki zilizochukuliwa na viongozi wa nchi ya Kenya katika kupambana na janga la korona. Msanii binti Salome anamtaja Raisi Uhuru Kenyatta kuwa alitoa tamko la kuzuia mikusanyiko, shule zote kufungwa hadi pale ufumbuzi wa namna ya kukabiliana na janga la korona ulipopatikana. Pia wimbo wa *"Corona Virus*" ulioimbwa na Inyenyeri group wakieleza kuhusu madhara yaliyotokea ikiwemo vifo vya watu wengi, na kuiasa jamii kumwomba Mungu aondo janga hilo. Aidha, mwonekano wa video ya wimbo huo inawaonyesha waimbaji wenyewe wakiwa wamevaa barakoa, na kukaa mbalimbali kama namna a kuendelea kuielimisha jamii kuepuka misongamano.

Kutokana na nyimbo kuwa na sifa ya mguso wa moyo hasa hisia za ndani alizanazo mtu, kwakupitia mifano ya nyimbo hizo tunaona namna ambavyo zinafikisha ujumbe wa moja kwa moja kwa wanajamii na kuendelea kuimba akilini mwao ilhali ukitoa mafunzo. Si hivyo tu, nyimbo au muziki hutumika kama tiba hasa kwa wagonjwa wa akili, wenye msongo wa mawazo, huzuni na upweke. Hili tunalithibitishwa katika utafiti uliofanywa na Mwalimu wa muziki daktari Aron Urio wa Chuo kikuu cha Dodoma kuhusiana na matibabu kwa njia ya muziki. Urio anaeleza kuwa mtu mwenye ugonjwa wa akili akisikizishwa mahadhi ya muziki wa taratibu wenye maudhui yanayohusu historia yake ya utotoni au historia yake kabla ya kuugua, anaweza kuvuta kumbukumbu na huweza kurejea katika utimamu wake wa akili. Urio anaendelea kueleza kwa kutoa mfano wa kisa cha Mfalme Sauli na Daudi katika Biblia Takatifu; 1Samweli16:23. Kisa hiki kinaonyesha namna ambavyo Mfalme Sauli alikuwa akipagawa na pepo na akili yake kuvurugika basi Daudi aliye stadi wakupiga kinubi alikuja mbele yake na kuanza kupiga kinubi huku akiimba kwa taratibu hadi ile hali ya kuchanganyikiwa iliyompata Mfalme Sauli inapoondoka hata akarudi katika urazini wake.

Vile vile mtu aliyepatwa na majonzi ya msiba au mambo ya kukatisha tamaa, akisikiliza nyimbo za faraja, hupata utulivu nafsini mwake. Kwa maneno hayo, tunaona wazi dhana ya fasihi simulizi kupitia utanzu wa nyimbo, unavyoweza kuwa nyenzo ya kitabibu kwa kufikisha tiba stahiki kwa wanajamii walioathiriwa na magonjwa.

Vilevile katika utanzu wa **mazungumzo**, tunapata mifano ya matangazo mbalimbali yanayorushwa kwenye runinga na kufikisha ujumbe wa kuitahadharisha jamii na kuielimisha kuhusu masuala ya afya. Mfano kipindi cha "ijue afya yako" huonesha midahalo, maswali na majibu kuhusiana na mambo mbalimbali yahusuyo afya ya binadamu. Kupitia kipindi hiki jamii imepata mafunzo mbalimbali kusuhu afya kama vile uzazi wa mpango, kansa ya shingo ya kizazi, tezi dume n.k. hapa tunaona jinsi ambavyo taaluma ya kitabibu kwa kutumia lugha rahisi na inayoeleweka kwa wanajamii huweza kuielimisha jamii kuhusu madhara ya magonjwa hayo na umuhimu wa kupima ili kujua afya yako. Aidha, matangazo mbalimbali katika vyombo vya habari huwa ni ya uhamasishaji wa upatikanaji wa huduma za kiafya kwa kuonyesha umuhimu wa kupima na kuijua afya yako ikiwa una maambukizi ya magonjwa au la. Kupitia matangazo ya mashirika ya bima za afya kama vile NSSF na NHIF hutangaza faida za kujiunga na kupata matibabu kwa urahisi kupitia usimulizi na maelezo yanayotolewa. Kwa mfano, shirika la PSI kupitia hisani ya Wamarekani hurusha matangazo yake katika runinga ya Taifa (TBC) kuhusu tahadhari mbalimbali za afya ya mama na mtoto, mama mjamzito na kutoa misaada na elimu wakati akikaribia kujifungua. Mfano mwingine ni kipindi cha "*Afya broadcast*" kinachorushwa katika Muhimbili TV kikiongozwa na Prof.Mohamed Janabi ambaye ni tabibu mbobevu wa masula ya moyo. Kipindi hiki huhusisha watu wawili wanaokuwa na mazungumzo kuhusu ugonjwa Fulani na namna ya kujikinga au kuchukua tahadhari. Vilevile huruhusu maswali kutoka kwa wasikilizaji au watazamaji. Ambayo husaidia uelewekaji wa magonjwa hayo na namna ya kuyadhibiti.

Hivyo basi, fasihi simulizi na tanzu zake imejidhihirisha waziwazi namna ilivyo vyenzo muhimi katka kufikisha ujumbe wa masuala ya afya kwa urahisi. Hii inaonyesha umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii na namna inavyoweza kuendana na wakati kwa kuakisi uhalisi wa mamboyanayotokea kwenye jamii.

**Mapendekezo**

Tunapotazama mustakabali wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake kwa miongo ijayo, hatunabudi kufanya yafuatato: Mosi, uimarishwaji wa uhusiano wa wanataaluma ya fasihi simulizi na taaluma ya kitabibu (afya) katika utendaji. Hii itasaidia kuingiza lugha ya Kiswahili katika taaluma ya kitabibu ili kurahisisha mawasiliano baina ya matabibu na wanajamii. Taaluma ya kitabibu hutegemea lugha ya kisayansi ambayo ni ngumu kueleweka kwa wanajamii wanaozungumza lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, taaluma ya utabibu ikitumia tanzu za fasihi simulizi, tunaona mafanikio zaidi katika kuielimisha jamii masuala ya afya.

Pili, uhusishwaji wa wataalamu wa fasihi simulizi katika uandaaji wa mada mbalimbali za kitabibu zinazokusudiwa kuifikia jamii. Jambo hili litasaidia urahisi wa utendaji katika sekta ya afya katika kuimarisha uhusiano wake na jamii husika.

Tatu, serikali za nchi zetu za Afrika Mashariki kuanzisha sera ya pamoja itakayomakinikia taaluma ya fasihi simulizi na kitabibu katika utekelezaji wa mpango wa ustawi wa jamii. Kwa kufanya hivyo, miongo ijayo tutarajie maendeleo katika nchi zetu. Pia wazungumzaji wa lugha ya kiswahili kwa jumla wataweza kupata elimu ya afya kwa urahisi na kupunguza maambukizi ya magonjwa. Kutokana na mjadala wa makala haya, tunatarajia kuona mwamko na ari mpya kwa wanataaluma wote wa lugha ya Kiswahili na fasihi, kuanza kuitazama fasihi simulizi na fasihi kwa jumla namna ya kuihusisha na taaluma zingine zilizopo kwenye jamii yetu katika kuleta maendeleo. Pia kuipa hadhi na thamani fasihi simulizi kutokana na mchango wake adhimu katika taaluma hii muhimu ya kitabibu.

**Hitimisho**

Kupitia ufafanuzi wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi na namna zinavyojipambanua katika kuhusika au kufikisha ujumbe wa kitabibu (afya) kwa jamii inatupa kuelewa ukamilishano uliopo katika taaluma ya kitabibu (afya) na fasihi. Aidha, ukamilishano huo unarahisisha ufikishwaji wa ujumbe na elimu ya masuala ya afya ambayo ni ya kisayansi.

Kwakutumia fasihi simulizi hususani tanzu zake, hatuna budi kuona kuwa ndiyo nyenzo muhimu inayotakiwa kuwekewa mkazo na sekta ya afya katika kufikisha ujumbe kwa jamii kwa wepesi na haraka.

Kwa jumla, fasihi simulizi inatoa njia madhubuti na za kipekee za kufikishia ujumbe wa afya kwa jamii. Kwa kutumia maigizo, masimulzi, mazungumzo, hadithi, methali, na nyimbo, fasihi simulizi inaweza kuwa chombo cha kuhamasisha mabadiliko chanya katika tabia na mitindo ya kiafya ya jamii. Hii ni kwa sababu fasihi simulizi ina uwezo wa kugusa hisia, kuelimisha, na kufundisha bila kuathiri umakini au kupuuza tamaduni za jamii husika. Jambo hili linawezekana kwani watu wote waliosoma na wasiosoma elimu ya darasani huielewa fasihi na sanaa kwa jumla.

## Marejeleo


Boas, F. (1942). *The mind of primitive man*. Macmillan.

Hann, C. (2021). One hundred years of substantivism economic anthropology.

Malinowski, B. (1945). *A scientific theory of culture and other essays*. North Carolina.

University of North Carolina Press.Mrikaria, S. (2007). Fasihi simulizi na technology mpya. Swahili forum 14: 197 – 2006.

Mulokozi, M.M (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mulokozi, M.M. (1983) "Utafiti wa Fasihi Simulizi" katika TUKI *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.: kur. 1-25.

Mushengezi, Aaron (2003), *Twentieth Century Literary Theory*, Makerere University, Kampala.

Njogu, K. & Wafula, R. (2007). Nadharia za uhakiki wa Fasihi. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi

Okphewho, I (1992). *African Oral Literature.*USA. Indiana University Press.

Radcliffe-Brown, A. R. (1947). *Social organization: Studies in the sociology of culture in relation to primitive communities*. Glencoe, IL. Free Press.

*Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hotuba ya Waziri wa Afya*
https://www.google.com/search?q=TAALUMA+YA+UTABIBU+PDF&ie=utf-8&oe=utf-8&client=firefox-b-ab (Imetembelewa tar. 18/6/2018)

TUKI (2007). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Oxford University Press. TUKI.

TUKI, (2003). *Fasihi.* Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. TUKI. Dar-es Salaam.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.